TANGAZO LA SERIKALI Na. 679 la tarehe 25/11/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MPANGO WA URASIMISHAJI WA ENEO LA IFUKUTWA YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Ifukutwa ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya urasimishaji.

Mpango wa kina wa eneo

3. Mpango wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

“Unaanzia kwenye alama P1 yenye majira - nukta 276334.14E, 9311155.98N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S85°19'37"E kwa umbali wa kilomita 0.703 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba P2 yenye majira - nukta 277035.08E, 9311098.68N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa N18°36'08"E kwa umbali wa kilomita 0.127 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba P3 yenye majira - nukta 277075.64E, 9311219.19N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S72°28'58"E kwa umbali wa kilomita 0.420 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P4 yenye majira - nukta 277476.17E, 9311092.77N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa N18°01'19"W kwa umbali wa kilomita 0.316 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P5 yenye majira - nukta 277574.12E, 9311393.81N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa N41°40'08"W kwa umbali wa kilomita 0.463 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P6 yenye majira - nukta 277266.07E, 9311739.94N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa N83°54'59"W kwa umbali wa kilomita 0.918 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P7 yenye majira - nukta 276352.42E, 9311837.31N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa S01°38'11"W kwa umbali wa kilomita 0.682 hadi ulipoanzia”.

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*